**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**
**SHULE YA SEKONDARI WANGING'OMBE**

Namba za Simu
Mkuu wa Shule 0762055083/0625157446
Makamu Mkuu wa Shule 0752161975
Matron/Patron: **0746980550**
Mwalimu wa Zamu: **0752380990**

SHULE YA SEKONDARI WANGING'OMBE
S.L.P 664
**MAKAMBAKO**
Tarehe 12/05/2023

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**S.L.P ……………………………………..**
**.........................................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WANGING'OMBE HALMASHAURI YA WANGING'OMBE MKOA NJOMBE MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule hii ipo Wilaya ya **Wanging'ombe** katika kijiji cha **Wanging'ombe** kando kando mwa Barabara kuu iendayo Mbeya(TANZAM HIGH WAY) ukitokea mji wa Makambako umbali wa kilometa 20. Kwa anayetokea Mbeya, Songwe, Dar es Salaam, Dodoma,Songea na kwingineko mahali pa kushukia ni Wanging'ombe Sekondari utaona kibao cha shule hapahitaji usafiri mwingine wowote ukishuka kibaoni. Aidha ukishukia Makambako utatakiwa kupanda daladala kwa nauli ya tsh.2,000 ambazo zipo mpaka saa moja na nusu usiku. .

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14.08.2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31.08.2023

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

- **WAVULANA.**
    - Mashati meupe mawili(2) ya mikono mirefu.
    - Suruali mbili RANGI YA BLUE BAHARI zenye mifuko miwili pembeni na mfuko mmoja nyuma YENYE TURN UP CHINI.(TAZAMA PICHA –KIAMBATANISHO) NA ISIWE MODAL.
    - Sweta mbili rangi dark blue( TAZAMA PICHA)
    - Soksi nyeusi jozi mbili au Zaidi.
    - Nguo za kazi suruali mbili rangi ya Khaki (TAZAMA PICHA) ISIWE MODAL
    - T-shirt 2 dark blue yenye kola.( TAZAMA PICHA) na isiwe na maandishi yoyote.
    - Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufunika miguu vya kamba visiwe na kisigino kirefu

- Vifaa vya michezo: Track suit blue bahari yenye mkanda mweupe,raba za michezo na jazzy nyekundu ya Liverpool yenye mikono mifupi.( TAZAMA PICHA).

➢ **WASICHANA.**

- Sketi mbili Blue Bahari **LAZIMA ZIFIKE CHINI YA MAGOTI kama ilivyo katika picha** sketi iwe ya linda box. Tazama picha iliyoambatanishwa.
- Mashati (2) meupe mikono mirefu. (Tazama picha iliyoambatanishwa)
- Sweta 2 rangi ni dark blue(Tazama picha iliyoambatanishwa)
- Soksi nyeupe jozi 2 au zaidi.
- Nguo za kazi sketi 2 rangi ya Khaki ( Tazama picha iliyoambatanishwa).
- T-shirt 2 rangi dark blue yenye kola.(Tazama picha iliyoambatanishwa).
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na kufunika miguu vya kamba.
- Vifaa vya michezo track suit moja blue bahari mkanda mweupe na raba za michezo na jazzy nyekundu ya Liverpool. ( TAZAMA PICHA).

**NB: KWA MWANAFUNZI WA KIKE WA KIISLAM ANARUHUSIWA KUVAA HIJABU NYEUPE na PIA AJE NA MTANDIO MWEUPE WA KUVAA NJE YA MASAA YA DARASANI**

## 2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i) Ream ya karatasi 2 (A4) kwa mwaka (iwe no. 1).

ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)

iii) Mashuka rangi ya bluu bahari 2, blanketi, mto na foronya rangi ya bluu bahari.

iv) Godoro aina ya Dodoma (2 ½ x 6).

v) Chandarua 2 ½ x 6.

vi) Sanduku la bati (Tranker) moja lakuhifadhia vitu vyake.

vii) Vyombo vya chakula, Chombo kikubwa cha kuhifadhia maji safi ya kunywa walau cha ujazo wa lita 5.

viii) Ndoo mbili ( za lita 10).

ix) Jembe moja lenye mpini.

x) Ufagio mmoja softboom wenye mpini(wavulana) na msichana alete mopper (drier) yenye mpini.

xi) Madaftali makubwa yakutosha kuanzia 8 (Counter books 4 quire).

xii) Nguo za ndani za kutosha;.

### Michango mbalimbali

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

***Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti Namba:***

***60601100017 NMB: Jina la Akaunti Wanging'ombe Sec School. Na uje Bank pay slip. Lipa kwa jina la Mwanafunzi na sio mzazi.***

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;


vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo uongozi wa shuleni;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII




Optatus Mng’ong’o
Mkuu wa Shule

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0762055083/0625157446**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752161975**
- **Mwandamizi Taaluma 0754586940**
- **Mwandamizi Malezi 0755 819172**

## FOMU NA.1 KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI.

**A: MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI…………………………………………………………………………………………
2. Shule ya "O"level uliyosoma……………………………………………………………………..
3. Namba ya mtihani ……………………………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………………………….
5. Nakubali nafasi niliyopewa/sitaki apewe mwingine (kata lisilohusika)
6. Nakiri/naahidi kutoshiriki migomo,fujo na makosa ya jinai
7. Sahihi ………………………………………………………………………..

**B: AFISA MTENDAJI**

JINA…………………………………………………………………………………………………………

KIJIJI/KATA…………………………………………..Wilaya ………………………….Mkoa……………………

Nathibitisha kuwa mwanafunzi …………………………………………………………ni mkazi wa kijiji/mtaa/kata hii na ni raia wa Tanzania.

Sahihi ……………………………………………Muhuri ……………………….tarehe …………………

**C: MZAZI/MLEZI**

JINA………………………………………………………………………………………………

Nakubali mwanafunzi apate Elimu yake hapo Wanging'ombe sekondari na kwamba atafuata sheria,kulipa ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule na vinginevyo aadhibiwe.

Pia atalelewa katika dini ya …………………………………………………………. **FOMU NA.2.**

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI.

JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………………………………

TAREHE YA KUZALIWA………………………………………………………………………………

JINSIA…………………………………………………………UMRI…………………………………………

MAHALI UNAPOISHI…………………………………WILAYA……………………………MKOA……………

SIMU NA………………………………………………………………………………………

JINA LA BABA……….……………………………………..YUPO HAI?...................................... JINA LA MAMA……………………………………………YUPO HAI?......................................

ANUANI ……………………………………………………………………………………… SIMU NA………………………………………………………….

KAZI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………………………………

**NB: TAARIFA ZA UONGO/ZISIZO SAHIHI ZITAPELEKEA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**



# FOMU NA.3. MEDICAL EXAMINATIONS.

**(To be completed by medical officer only)**

1. Pupil's name …………………………………………………………………………………………….
2. Age……………………………………………………………………………………………………..
3. Blood count (white and red)……………………………………………………………………….
4. Stool examination ……………………………………………………………………………………..
5. Syphilis or/and other venereal diseases test ……………………………………………………
6. T.B test ………………………………………………………………………………………………………..
7. Eye test ………………………………………………………………………………………………………..
8. Ears ……………………………………………………………………………………………………………..
9. Abdomen ……………………………………………………………………………………………………

10. 10. Spleen ………………………………………………………………………………………………………..

11. Urine for plamo test ……………………………………………………………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION**


If any e.g physical defeats, impairment, infections, pregnancy, chronic or family diseases etc

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

**I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION**

STATION……………………………………………………………………………………SIGNATURE………………………….

DATE…………………..DESIGNATION…………………………………OFFICIAL STAMP……………………………..



**FOMU NA.4. PLEASE IF POSSIBLE COME WITH THE FOLLOWING BOOKS/REFERENCE/MATERIALS RELEVANT TO YOUR COMBINATION AS LISTED BELOW.**

1. **HISTORY**
   - i. Essentials in Advanced Level History Paper 1&2 ………. By Saleh Yassin
   - ii. Major events in African History …………………………by Mwijage
   - iii. Africa since 1800- 4th edition iv. The marking of modern Africa
   - v. How Europe under develop Africa
   - vi. Europe from 1815 ……………by Peacock
2. **Geography**
   - i. Certificate of Geography (oxford) …….by mary Mugo.Robert Kamugat and Paul kibuuka
   - ii. General Geography in diagrams ………………… by R.B bunnet
   - iii. Photography interpretation and elementary surveying for secondary A level iv. Certificate human and economic Geography ……..by Morgan and Leong Ghang
   - v. Physical geography by D.T Msabila
3. **English Language**
   - i) English language I by Asheri N.
   - ii) Advanced learner's dictionary by oxford 10th edition

     Plays
     - i) I will mary when I want -Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii
     - ii) An enemy of the people- Henrick Ibsen

     Novels & short stories
     - i) Beautiful ones are not yet born – Anyi kwei armah ii) A man of the people…….. Chinua Achebe

     Poetry
     - i) Selected poems – Institute of education
4. **General Studies**

   i) Understanding advanced level general studies by J.Bigirwamungu $ S.Deogratius ii) General Studies Notes ( for A-level form V-Vi)……..By Mshiu and Nyangwine
5. **Kiswahili**
   - **I.** lugha na sarufi …..TIE.
   - **II.** Nadharia ya lugha 5&6 ….Nyambari **III.** Kiswhili kidato cha 5&6 …oxford.
   - **IV.** Tahakiki kidato 5&6
   - **V.** Kiswahili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzikidato cha tano na sita (Fasihi)

   **Ushairi**
   - i. Kimbunga …………..G.Gorn (TUKI) 1994
   - ii. Changu Tamu ……….T.A Mvungi
   - iii. Mapenzi Bora ………… S. Robert

**Riwaya**
- i. Vuta N'kuvute ……………Shafi A Shafi
- ii. Kufikirika ……………………S.Robert
- iii. Mfadhili ……………………..Hussein Tuwa
- iv. Usiku utakapokwisha…………Mbunda Msokile

**Tamthilia**
- i. Morani ……. E Mbogo
- ii. Kivuli kinaishi ………….. Said Mohamed
- iii. Kwenye ukingo wa Thim ………. E Hussein iv. Nguzo mama ………………………. (DUP) 1982.

A. **<u>SARE YA WASICHANA.</u>**

**PICHA 1. SARE YA DARASANI PICHA 2. SARE YA KUSHINDIA NJE YA DARASA. PICHA 3. SARE YA MICHEZO . PICHA 4. SWETA LA SHULE PICHA 5. TRACKSUIT.**


**1 2 3 4**

**5**















B. **<u>SARE YA WAVULANA</u>**

**PICHA 1- SARE YA DARASANI SHATI JEUPE MIKONO MIREFU, PICHA 2. SARE YA KUSHINDIA NJE YA DARASANI PICHA 3 SWETA LA SHULE, PICHA 4 NI SARE YA MICHEZO, NA PICHA 5. TRACKSUIT.**

**1 2 3 4 5**















**SHATI JEUPE MIKONO MIREFU**

## ANGALIZO KUU.

**1. NI MARUFUKU SURUALI KUWA YAKUBANA CHINI. (MODAL STYLE) 2. SKETI NI LAZIMA IWE NDEFU SANA KAMA MCHORO ULIVYO AU ZAIDI.**

**2. Namba ya simu ya shule mwanafunzi awapo shuleni ni *<u>0752380990</u>* wakati wote namba hii itakuwa na mwalimu wa Zamu.**